# Twende Pamoja

## HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

Toleo maalum la Kampeni ya Afya na Usafi wa mazingira 2016

**Ndani**

Watendaji Kata na Vijiji watakiwa kuhimiza Kampeni ya afya na usafi wa mazingira
Uk.6





**Habari katika picha**
**Uk 11&12**

# Fahamu Kampeni ya Afya Na Usafi wa Mazingira inavyotekelezwa katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.



*Moja ya vyoo bora na vyakisasa ambavyo vimejengwa kupitia programu ya SWASH katika shule ya msingi Idongela kata ya Ikuna ikiwa ni utekelezaji wa kampeni ya afya na usafi wa mazingira katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.Ujenzi wa vyoo hivi umekwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya maji.*



Utekelezaji wa Kampeni ya afya na usafi wamazingira kuanzia ngazi ya kaya

Uk.....3





*Wataalamu wa idara ya afya wakiwakatika ukaguzi wa ujenzi wa vyoo bora katika Kata ya Ikuna.Ukaguzi wa mara kwa mara hufanyika pamoja na kutoa elimu kwa wananchi.*

Linatolewa na Ofisi ya

Mkurugenzi Mtendaji,

Halmashauri ya Wilaya

Njombe.

S.L.P 547 Njombe.

Phone: 026 2782111

Fax: 026 2782857

Email:ded@njombedc.go.tz

info@njombedc.go.tz

njombedc@yahoo.com

Tovuti:www.njombedc.go.tz

## WOSIA WA SARA DUMBA

"Tanzania bila kipindupindu inawezekana, zuia maambukizi mapya kwa kuzingatia usafi wa mazingira", Tunatakiwa kutekeleza kwa vitendo kauli hii kwa kuhakikisha kuwa sisi pamoja na jamii inayotuzunguka tunadumisha hali ya usafi wa mazingira. Hili litawezekana tu kama sisi viongozi tutakuwa makini katika kusimamia, kuhamasisha na kufuatilia kwa ukaribu mkubwa utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira katika maeneo tunayoyasimamia. Hakika hili linawezekana, kila mmoja wetu anatakiwa kuthubutu na kuchukua hatua madhubuti"

# Ijue kampeni ya Afya na Usafi wa Mazingira

Kampeni ya Kitaifa ya afya na usafi wa mazingira nchini Tanzania ilizinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 05 Juni 2012 mjini Moshi Mkoani Kilimanjaro.

Kampeni hii ililenga kuinua kiwango cha upatikanaji wa huduma bora za usafi wa mazingira kwa kuhakikisha kuinua uwiano wa kaya zenye vyoo bora kwa zaidi ya asilimia 50% hadi kufikia mwaka 2015.

Kampeni hii ililenga kupunguza kuenea kwa magonjwa yasababishwayo na mazingira machafu (Sanitation related diseases).

Kampeni hii kwa awamu ya kwanza imetekelezwa katika ngazi ya kaya na katika shule za msingi na ililenga kuhakikisha kuwa kila kaya katika eneo la kampeni inakuwa na vyoo bora pamoja na miundombinu ya kunawa mikono baada ya kutoka chooni.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kampeni hii inatekelezwa katika kata zote 12, vijiji 45 na vitongoji 227. Pia kampeni hii inatekelezwa katika shule zote 52 za msingi. Katika ngazi ya jamii/ kaya mambo yafuatayo yamefanyika

Kutoa mafunzo kwa viongozi wa Halmashauri (Wajumbe wa DCC, Baraza la madiwani, wakuu wa idara pamoja na wadau mbalimbali waliopo katika halmasahuri yetu)

Kutoa mafunzo kwa timu ya usimamizi wa kampeni ngazi ya Wilaya ikijumuisha wataalam kutoka idara ya Afya, maji, elimu msingi na maendeleo ya Jamii

Kutoa mafunzo ya utekelezaji wa kampeni kwa viongozi wa kata, vijiji na vitongoji vyote pamoja na wahudumu wa afya katika vijiji vyote vya kampeni

Kukusanya takwimu za usafi wa mazingira na kuziingiza katika rejista maalum za kitongoji

Kufanya mikutano ya uhamasishaji (uchefuaji) katika vitongoji vyote 227 vilivyopo katika Halmashauri

Kutoa mafunzo kwa mafundi ujenzi juu ya ujenzi wa vyoo bora

Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuona maendeleo ya utekelezaji wa kampeni hii.

Kufanya vikao mbalimbali vya tathmini ya utekelezaji na kubadilishana uzoefu kati ya viongozi wa vitongoji, vijiji, kata, Wilaya na wadau mbalimbali wa usafi wa mazingira katika Halmashauri.




*Pamoja na kujenga vyoo wataalamu wa Halmashauri hupita kukagua kama ujenzi umekidhi viwango vilivyowekwa na Serikali. Wataalamu wa Halmashauri wakiwa katika ukaguzi wa vyoo vilivyojengwa katika shule ya Msingi Lole Ikuna katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*

# SHULE ZA MSINGI

Kampeni hii imekuwa pia ikitekelezwa kwa mafanikio makubwa kwenye shule za msingi na yafuatayo yamefanyika hadi sasa

1. Kutoa mafunzo kwa viongozi wa vijiji pamoja na kamati za shule juu ya mwongozo mpya wa SWASH
2. Kutoa mafunzo kwa walimu wa afya juu ya utekelezaji wa program ya SWASH
3. Kutoa mafunzo na kuanzisha klab za SWASH katika shule za msingi
4. Kukarabati/ kujenga vyoo bora katika shule za msingi kwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa katika miongozo ya utekelezaji wa kampeni.
5. Kuhakikisha uhakika wa upatikanaji wa maji shuleni kwa kujenga matenki ya kuvuna maji ya mvua, kuchimba visima au kusogeza maji shuleni
6. Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara shuleni ili kuona utekelezaji wa kampeni.

## Mafanikio yaliyopatikana

1) Idadi ya kaya zenye vyoo bora imeongezeka kutoka asilimia 3% mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 84% mwezi April 2016.
2).Tumefanikiwa kuvuka malengo ya millenia yanayotaka kila Halmashauri kufikia angalau asilimia 50% ya vyoo bora ifikapo mwaka 2015
3). Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imekuwa ikitekeleza kwa ufanisi kampeni hii katika ngazi ya mkoa na taifa hali iliyopelekea kuwa mshindi wa kwanza katika utekelezaji wa kampeni hii kwa mwaka 2015.
4) Halmashauri imefanikiwa kuwa na vijiji 25 vilivyokamilisha kampeni hii kwa asilimia 100% (yaani kaya zote katika vijiji hivyo zimejenga vyoo bora kwa mujibu wa sifa za kampeni na kila kaya ina sehemu ya kunawa mikono). Vijiji hivyo vipo katika hatua mbalimbali za kupewa hati ya ODF.
5) Wadau mbalimbali kama vile UNICEF, mashirika yasiyo ya kiserikali ya PDF, IECA na SHIPO pamoja na taasisi mbalimbali za kijamii na dini wameonesha nia za kuiunga mkono Halmashauri ili kuhakikisha kuwa mpaka kufikia mwaka 2016, Halmashauri nzima ya Wilaya ya Njombe inakuwa na vyoo bora kwa asilimia 100%
6) Viongozi wote wa Halmashauri wakiongozwa na mkuu wa Wilaya pamoja na Mkurugenzi wamekuwa wakifanya ziara kuhamasisha utekelezaji wa kampeni katika vijiji mbalimbali. Hali hii imetoa mwamko mkubwa kwa jamii kutekeleza kampeni na pia viongozi wengine kufuatilia kampeni kwa ukaribu. Pia madiwani ambao ni wajumbe wa kamati ya kudumu ya Huduma za Jamii (Elimu, Afya na Maji) wamekuwa wakifuatili kwa ukaribu utekelezaji wa kampeni kwani taarifa za utekelezaji wa kampeni huwasilishwa katika kamati hii kila robo
7) Halmashauri imefanikiwa kuanzisha siku maalumu ya usafi wa mazingira ambayo ni kila Jumamosi ya mwisho ya mwezi. Wataalam hutumia siku hii kuelimisha jamii kuhusu masuala ya usafi wa mazingira kwa kutumia njia za radio, matangazo, mabango pamoja na vipeperushi. Watu sasa wana uelewa juu ya kampeni
8) Halmashauri ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya mpango mkakati wa kuinua kiwango cha huduma bora za maji na usafi wa mazingira (water and sanitation strategic plan). Mpango huu umeandaliwa na Halmashauri kwa



*Afisa afya wa Halmashauri ya wilaya ya Njombe Remigius Sungu akigawa zawadi kwa wanafunzi wa shule ya Msingi Lole ambao wako katika Club za SWACH ambazo zimekuwa zikihamasisha kwenye Kampeni ya afya na usafi wa mazingira kwenye Shule*

Uk 5

Uk 4

Mpango huu umeandaliwa na Halmashauri kwa ufadhili wa UNICEF

9) Halmashauri imepanga kuhakikisha kuwa inakamilisha utekelezaji wa kampeni hii kwa ngazi ya kaya kwa asilimia 100% ifikapo mwezi Juni 2017. Jambo hili litawezekana kutokana na ushirikiano tunaoupata kutoka kwa viongozi wa ngazi za juu kuanzia DC, DED pamoja na wanasiasa (madiwani). Pia viongozi wa kat, vitongoji na vijiji husika watahusishwa kikamilifu

10) Baadhi ya vijiji na kata kujiwekea sifa za ziada za vyoo bora ili kuitekeleza kampeni hii kwa ufanisi zaidi. Baadhi ya maeneo wamekubaliana kuwa vyoo vinavyojengwa ni lazima vijengwe kwa tofali na kuezekwa kwa bati. Pia baadhi wamekubaliana kuwa ujenzi wa vyoo ni lazima uende sambamba na ujenzi wa bafu



*Kamati ya afya ya Kijiji cha Wanginyi Kata ya Matembwe Halmashauri ya wilaya ya Njombe wakitoa ushaurikwa Bibi Semwenda ikiwa ni moja ya majukumu yao ya kuhimiza usafi wa mazingira kwa kutoa elimu kwa wanakijiji.*

> "Ni wajibu wa viongozi na kila kaya kuhamasishana kuhusu umuhimu wa Kampani ya Afya na Usafi wa Mazingira."

# CHANGAMOTO

Pamoja na Halmashauri ya wilaya ya Njombe kutekeleza kwa mafanikio Kampeni ya afya na usafi wamazingira bado katika utekelezaji wa kampeni hii kumekuwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo

1) Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa kampeni hii

2) Kuchelewa kufika kwa fedha za kampeni hali inayopunguza kasi ya utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea. Hali hii husababisha wataalam kufanya kazi kwa kujitolea na hivyo kupunguza kasi ya utekelezaji

3) Ukosefu wa vyombo vya usafiri (magari na pikipiki) kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa kampeni. Hali hii imekuwa ikiwapa mzigo mkubwa sana kwani hulazimika kutumia usafiri wa mabasi na pengine kutembea umbali mrefu kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa kampeni.

4)Kutokutosheleza kwa fedha za kampeni na hivyo kufanya utekelezaji wa shughuli hizi kuwa mgumu.

5.)Kutokutosheleza kwa miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa kampeni pamoja na rejesta kwa ajili ya kutunzia takwimu za utekelezaji wa kampeni hii.

Halmashauri itaendelea kutumia rasilimali chache zilizopo katika kuhakikisha kuwa kila kaya inakuwa na choo bora ifikapo mwezi Juni 2017.

Pia tunaiomba Mkoa na wizara kuhakikisha kuwa miongozo kwa ajili ya utekelezaji wa kampeni hii inapatikana kwa wakati ili kuwezesha kufanyika kwa shughuli zilizopangwa kwa ufanisi.

# MKURUGENZI AWAAGIZA VIONGOZI WA KATA NA VIJIJI KUSIMAMIA KAMPENI YA USAFI WA MAZINGIRA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Hajjat Farida Mwasumilwe amewataka viongozi wote wa Kata na vijiji kusimamia kikamilifu kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira katika maeneo yao.

Akizungumza katika kikao cha Watendaji wa Kata na Vijiji alisema kumekuwa na uzembe katika kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika maeneo ya Kata na Vijiji na kumtaka kila kiongozi kuhakikisha anasimamia kwa ukamilifu kampeni ya usafi wa mazingira katika eneo lake na atakayezembea atachukuliwa hatua.

"Haiwezekani kuwavumilia watu wanaohatarisha afya zao na za jamii kwa ujumla kwa kukataa kujenga vyoo bora katika kaya zao, sheria ipo wazi kabisa juu ya watu kama hawa nawaagiza maafisa watendaji wote mkashirikiane na maafisa afya kutokomeza tabia hii katika maeneo ynu ya kiutawala"alisema Bi Hajjat Mwasumilwe.

Alisisitiza kuwa Suala la kuwa na choo bora ni amri na sio hiari na hakuna kiongozi anayependa kuongoza watu wasio na afya bora. "kawaambieni watu wenu kuwa asiyetaka kujenga choo bora basi ahame katika Halmashauri yetu kwani watu wasio na vyoo bora siku zao zinahesabika na viongozi wanaowafuga watu hao pia siku zao zinahesabika" aliongeza Bi Hajjat Mwasumilwe.



*Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Bi Hajjat Farida Mwasumilwe akitoa maelekezo kwa wataalam wa Halmashauri ya Wilaya katika moja ya ziara yake ya kuzungumza na wataalamu juu ya masuala mbalimbali ikiwemo Kampeni ya afya na usafi wa mazingira.*



"Hayati Sara Dumba alikuwa mstari wa mbele kwenye kuhamasisha kampeni ya afya na usafi wamazingira tumuenzi kwa vitendo kwa kuweka safi mazingira yetu. "

# YAJUE MASHINDANO YA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA

Mashindano ya Afya na Usafi wa mazingira ni mkakati wa kitaifa wenye lengo la kuleta mabadiliko ya tabia pamoja na kuongeza ushirikishwaji wa jamii na wadau mbalimbali katika kuinua kiwango cha Afya na usafi wa mazingira na hatimaye kupunguza kuenea kwa magonjwa yatokanayo na mazingira machafu. Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 60 ya magonjwa yote yanayoripotiwa hutokana na mazingira machafu.

Mashindano haya hufanyika kila mwaka na huhusisha vijiji, kata na shule zote zinazotekeleza kampeni ya usafi wa mazingira. Uhakiki wa mashindano haya hufanywa na timu ya wataalam wa Wilaya wakiongozwa na Afisa Afya wa Wilaya ambaye ndiye mratibu wa kampeni hii. Baadaye mkoa nao hushindanisha Halmashauri zake ili kupata washindi ambao husindanishwa na washindi kutoka mikoa mingine ili kupata washindi wa jumla kimkoa katika utekelezaji wa masuala ya afya na usafi wa mazingira.

Washindi wa mashindano haya hupata zawadi mbalimbali wakati wa kilele cha maadhimisho ya siku ya mazingira duniani ambayo hufanyika kila tarehe 05 June kila mwaka.

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imekuwa ikishiriki kwa mafanikio makubwa na kupata ushindi katika mashindano haya katika ngazi ya kimkoa na kitaifa. Kwa mwaka uliopita Halmashauri yetu ilishika nafasi ya kwanza Kimkoa na nafasi ya kwanza kitaifa katika mashindano haya ambayo huratibiwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.



*Wanafunzi wa shule ya msingi Wanginyi wakinawa mikono baada ya kutoka chooni.Kampeni hii imesaidia wanafunzi kuzingatia usafi na kuepukana na magonja ya mlipuko.*

## LENGO KUU

Lengo kuu la mashindano haya ni kuhamasisha wilaya, kata na vijiji ili viweze kuongeza jitihada za kuinua kiwango cha Afya na usafi wa mazingira kuanzia ngazi ya kaya na jamii na hatimaye kupunguza kuenea kwa magonjwa yatokanayo na mazingira machafu.

## MALENGO MAHSUSI

Kuongeza ufahamu na uelewa ndani ya jamii kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi wa mazingira.

Kuzuia magonjwa ya kuambukiza, vifo na madhara mbalimbali yanayotokana na magonjwa yatokanayo na mazingira machafu.

Kuiwezesha jamii kubadili tabia na mazingira wanamoishi na kuzingatia usafi na kanuni bora za Afya

Kuongeza uwajibikaji kwa watendaji wote wa ngazi ya wilaya, kata na vijiji pamoja na wadau wengine katika jamii kuzingatia suala zima la usafi wa mazingira kuwa ni jukumu lao.

"Kila mtu kwa nafasi yake akiwajibika kipindupindu kitakuwa Historia Katika Halmashaui ya wilaya ya Njombe".

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE YAANDAA SHERIA NDOGO ZA KUSIMAMIA USAFI WA MAZINGIRA

Sheria ndogo hizi zitajulikana kama sheria ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe 2016 na zitaanza kutumika baada ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali

Sheria hizi zinatoa maelekezo ya mambo mbalimbali ya usafi wa mazingira kwa kuainisha wajibu mbalimbali katika;

i) Wajibu wa kuhakikisha mazingira yanakuwa safi wakati wote

ii) Ukusanyaji na uhifadhi wa taka ngumu

iii) Kuzuia uriririshaji wa maji machafu ovyo

iv.) Wajibu wa kaya na jamii kwa ujumla kuhakikisha kuwa wanakuwa na vyoo bora

v.) Wajibu wa kila jamii na taasisi kuhakikisha kuwa vyoo vyao vinakuwa na miundombinu ya kunawa mikono pamoja na kuhakikisha kuwa vyoo hivyo vinatunzwa vizuri wakati wote

Sheria hiyo pia imeainisha adhabu na faini mbalimbali kwa wanaokiuka kanuni za usafi wa mazingira ikiwa ni faini isiyopungua 50,000/= au kifungo cha miezi 6 au vyote viwili kwa pamoja .

Sheria hii pia imetoa maelekezo ya namna jamii inavyotakiwa kuchangia gharama mbalimbali za uzoaji wa taka.

## Gharama mbalimbali za uzoaji wa taka

| 1 | AINA YA BIDHAA | ADA KWA MWEZI |
|---|---|---|
| 2 | Baa na Maduka ya vinywaji (Groceries) | 3,000/= kwa mwezi. |
| 3 | Migahawa na Mama Lishe | 3,000/= kwa mwezi. |
| 4 | Nyumba za Wageni | 3,000/= kwa mwezi. |
| 5 | Kumbi za Starehe na Saluni | 3,000/= kwa mwezi. |
| 6 | Viwanda vikubwa | 5,000/= kwa mwezi. |
| 7 | Viwanda vidogo vidogo | 3,000/= kwa mwezi. |
| 8 | Majengo mengine ya biashara | 3,000/= kwa mwezi. |
| 9 | Mafundi seremala na Gereji | 2,000/= kwa mwezi. |
| 10 | Wachoma chipsi, Kuku,Nyama | 3,000/= kwa mwezi. |
| 11 | Wauza mbao | 3,000/= kwa mwezi. |
| 12 | Vioski | 3,000/= kwa mwezi. |
| 13 | Nyumba za kuishi | 1,000/= kwa mwezi. |

"Jenga tabia ya kutupa taka kwenye shimo na kufanya usafi kwenye maeneo unayoishi ili kuepukana na magonjwa ya mlipuko ikiwemo kiindupindu".

# KLAB ZA USAFI WA MAZINGIRA SHULENI (SCHOOL WASH CLUBS)

Katika kutekeleza kampeni ya afya na usafi wa mazingira shuleni kupitia program ya SWASH Halmashauri imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali na namna shughuli za SWASH zinnavyotakiwa kufanyika. Mojawapo ya mafunzo haya ni mafunzo ya uanzishaji wa klabu za usafi wa mazingira shuleni (School WASH clubs) ambazo zina majukumu mbalimbali ya kuhakikisha kuwa mazingira ya shule yanakuwa safi wakati wote. Klabu hii hutumia njia ya mtoto kwa mtoto kufikisha elimu mbalimbali ya afya kupunguza magonjwa yanayosababishwa na uchafu wa mazingira kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo

1) Maji safi na salama
2) Usafi binafsi
3) Uandaaji na utunzaji salama wa chakula na ulaji salama
4) Usafi wa Mazingira kwa ujumla
5) Matumizi sahihi ya vyoo katika shule na katika jamii

## Mafunzo haya huwa na malengo yafuatayo

1.)Kumjenga mtoto katika tabia nzuri za usafi
2) Kutoa ujumbe wa afya katika jamiii kupitia watoto wa shule kwa mabadiliko
3) Kuwasaidia watoto kujenga na kuwa na furaha na kujifunza vizuri
4) Kuongeza uelewa wa wafanyakazi wa afya katika jamii na uhusiano na watoto wa shule

## Wajibu wa mwanachama wa klabu WASH shuleni

Kuwapata wanachama watakaojitolea kwenye klabu ya WASH.
1) Kuwafundisha wanachama na wanafunzi wengine masuala ya maji na usafi wa mazingira
2) Kuwafahamisha wanajamii wa shule kufanya usafi, kupanda miti na kazi zingine nzuri.
3) Kukagua pointi za maji, vyoo, uoshaji mikono na mazingira kwa ujumla.
4) Kutengeneza program za kukusanya pesa ili kuwa na mfuko ili kujenga vifaa, kununua sabuni
5) Kutengeneza program mbalimbali na kuzifikisha katika jamii. program hizo zinaweza kuhusiana na:
1) Kampeni ya usafi
2) Kusafisha vyanzo vya maji
3) Kuvilinda vyanzo vya maji kutokana na mafuriko, wanyama n.k

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kuna Jumla ya shule za msingi 52 ambapo jumla ya shule 38 sawa na asilimia 73% zimefanikiwa kuwa na klab hizi. Jitihada za kuhakikisha kuwa shule zote zinakuwa na klabu hii zinaendele kufanyika.





Afisa afya wa Hamashauri Remigius Sungu akitoa zawadi kwa Clab za SWASH katika shule ya Msingi Kitole ikiwa ni motisha kwa klabu hizi katika kuelimsha wanafunzi wanzao juu ya usafi wa mazingira. Kulia watoto wakipata chakula baada ya kupata elimu juu ya kampeni ya afya na usafi wa mazingira

# Njombe watekeleza kwa vitendo agizo la Rais Magufuli

Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imetekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr John P Magufuli la kuitumia tarehe 9 Disemba 2015 kufanya usafi wa mazingira ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya uhuru wa Tanganyika.

Katika kutekeleza agizo hilo kila Kata imefanya shughuli za usafi wa mazingira katika taasisi za umma zikiwemo zahanati, shule za msingi na sekondari, maeneo ya biashara pamoja na maeneo ya wazi pamoja na kwenye kaya.

Uzinduzi wa maadhimisho ya usafi wa mazingira ulifanywa na mbunge wa jimbo la Lupembe ambalo liko katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Bw Joram Ismael Hongoli kwa kufanya usafi katika ofisi za Halmashauri hiyo zilizopo mjini Njombe.

Kiwilaya kilele cha maadhimisho ya uhuru kilifanyika katika Tarafa ya Lupembe ambapo mgeni rasmi alikuwa ni hayati Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Bi Sarah Dumba "Tanzania bila kipindupindu inawezekana, zuia maambukizi mapya kwa kuzingatia usafi wa mazingira", Tunatakiwa kutekeleza kwa vitendo kauli hii kwa kuhakikisha kuwa sisi pamoja na jamii inayotuzunguka tunadumisha hali ya usafi wa mazingira. Hili litawezekana tu kama sisi viongozi tutakuwa makini katika kusimamia, kuhamasisha na kufuatilia kwa ukaribu mkubwa utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira katika maeneo tunayoyasimamia. Hakika hili linawezekana, kila mmoja wetu anatakiwa kuthubutu na kuchukua hatua madhubuti" ambaye aliwaongoza viongozi mbalimbali wa Wilaya ya Njombe pamoja na wananchi kufanya usafi katika kituo cha afya Lupembe.

Akizungumza na viongozi pamoja na wananchi walioshiriki zoezi hilo Bi Dumba aliwataka viongozi na wananchi kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu ya maadhimisho ya siku ya uhuru mwaka huu inayosema Tanzania bila kipindupindu inawezekana, zuia maambukizi mapya kwa kuzingatia usafi.

"Tunatakiwa kutekeleza kwa vitendo kauli hii kwa kuhakikisha kuwa sisi pamoja na jamii inayotuzunguka tunadumisha hali ya usafi wa mazingira, Hii itawezekana tu kama sisi viongozi tutakuwa makini katika kusimamia, kuhamasisha na kufuatilia kwa ukaribu mkubwa utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira katika maeneo tunayoyasimamia." Alisema bi Dumba.

Amewataka wananchi kuendelea na suala la usafi wa mazingira kwa muda wote badala ya kusubili maadhimisho pekee.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Bw Paulo Malala, alimuhakikishia mkuu wa Wilaya ya Njombe kuwa kipindupindi hakiwezi kutokea katika Halmashauri hiyo.

Alisema kuwa Halmashauri ya Njombe imejipanga vizuri katika suala la usafi wa mazingira kutokana na kuwepo kwa kampeni ya afya na usafi wa mazingira ambapo Halmashauri ya wilaya ya Njombe ni miongoni mwa Halmashauri zinazotekeleza kampeni huyo.

Bw Malala alisema kupitia kampeni hiyoelimu juu ya usafi



aliyekuwa Mkuu wa wilaya ya Njombe hayati Bi Sara Dumba akipanda maua katika kituo cha afya Lupembe enzi za uhai wake ikiwa ni moja ya sehemu ya kuhimuza usafi wa mazingira.



Mkurugenzi mtendaji wa Halmashauri ya Njombe (sasa Kasuru) akikwatua uwanja ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku ya Uhuru ambayo iliazimishwa kwa kufanya usafi.





*Elimu wanayopewa watoto katika Shule kuhusu umuhimu wa usafi baada ya kutoka chooni imewasaidia. Miundombinu bora ya maji huwawezesha wanafunzi kuwa katika hali ya usafi na hivyo kuepukana na hatari ya kupata magonjwa ya milipuko.Pichani wanafunzi wa shule ya Msingi Sovi wakinawa mikono baada ya kutoka chooni. Kulia ni miundombinu ya maji shule ya Msingi Wanginyi.*





*Ukaguzi wa vyoo na miundo mbinu yake mara kwa mara unaofanywa na wataalamu wa Halmashauri kwa kushirikiana na madiwani husaidia kuimarisha usafi wa mazingira.Pichani Kamati ya Afya kijiji cha Wanginyi wakifanya ukaguzi wa vyoo kwenye ngazi ya jamii. Kulia madiwani na wataalamu wakifanya ukaguzi kwenye vyoo katika Shule ya Msingi Kidegembye.*





*Elimu imekuwa nguzo muhimu katika kufanikisha Kampeni ya afya na usafi wa mazingira Katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe.Pichani Kulia Kamati ya afya wakitoa elimu kwa bi mwenda (69) katika kijiji cha Wanginyi.Kulia afisa Afya Halmashauri ya wilaya Njombe Bw Remigius Sugu akitoa zawadi ya vifaa vya michezo kwa kwa wanafunzi wa shule ya msingi Ukalawa ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wa kampeni ya afya na usafi wa mazingira mwaka 2015.*




*Ujenzi wa vyoo bora na vya kisasa kwenye shule za msingi  Isitu Ninga unawahakikishia wanafunzi afya. Pichani kushoto choo cha zamani na kulia ni choo kipya kilichojengwa chini ya programu ya afya na usafi wa mazingira.vyoo hivi vimezingatia watu wenye mahitaji maalumu*




*Ujenzi wa vyoo bora na vya kisasa katika shule za msingi za Halmashauri ya wilaya ambazo zinatekeleza Kampeni ya afya na usafi wa mazingira umekwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya maji ili kuimarisha usafi na kuondokana na magonjwa ya milipuko.Pichani kulia na kisima cha maji katika shule ya Msingi  Havanga na kushoto tank la kuhifadhia maji katika Shule ya Msingi Ninga.*





*Katika eneo la ngazi ya vijiji na vitongoji wananchi wamehamasika kujenga vyoo bora vya masinki pamoja na kuweka vibuyu chilizi. Pichani ni Bi mwenda akinawa kwa kutumia Kibuyu chirizi baada ya kutoka chooni katika Kijiji cha Wanginyi  Kata ya Matembwe Halmashauri ya Wilaya Njombe.*